Zao Tatu Mhimu
(Three Important Births)

Na

John Kombo

Zao Tatu Mhimu
(Three Important Births))

Na

John Kombo

July 9, 2013

Zao Tatu Mhimu

"Uzao Wa Asili"

Hivi ndivyo nilivyokuja katika ulimwengu huu. Nilizaliwa kimwili. Nikiwa na wazazi wawili – baba yangu Charles Nandwa, na mama Jeskah Nandwa. Mungu akaamua kwamba sheria ya uzazi uwe njia ya kupitia kuingia katika ulimwengu huu na ndivyo nilivyokuja katika ulimwengu huu wa kimwili kwa uzao wa asili.

Kabla sijakuwa mtu mzima na kutambua matendo yangu katika uhusiano na sheria ya Mungu (umri wa kuhesabika), nilikuwa msafi kama Ufalme wa Mungu. Yesu alisema, "*msipoongoka mkawa kama watoto wadogo, hamwezi kuingia katika ufalme wa Mbinguni.*"

Nilipofikia umri mkubwa, baba yangu alinipeleka shuleni. Nilikutana na watoto wengine pale na baadhi wakawa rafiki zangu. Nilianza kuwa na ujuzi wa dunia hii ambayo sikugundua kama imeundwa kwaajili ya uharibifu. Nilielendelea katika maisha ya shule, ilikuwa ni nzuri na kufurahisha, kwanzia shule ya msingi hadi sekondari (kidato cha nne); toka hapo nikaenda katika chuo cha waalimu ambapo nilisomea ualimu wa shule ya msingi.

Nilihitimu chuo na kuanza kufundisha. Nilipata fedha; fedha hiyo ikanifikisha sehemu ambapo ni hatari, kwa sababu nilianza kulewa na kufanya kila aina ya dhambi ambayo pesa yangu iliniongoza kama vile, wanawake, kucheza mziki, n.k.

Siku moja niliingia katika shida; nilivamiwa na majambazi nilipokuwa nikirudi nyumbani usiku. Karibia nipoteze maisha yangu, lakini nilipoteza pesa zangu zote.

Mtume Paulo anatoa maelezo ya maisha niliyoishi katika kitabu cha Waefeso Sura ya 2:

- "*Walipokuwa wangali wenye dhambi, walikufa*" (ms 1-2). Nilikuwa mfu ingawa nilikuwa hai.
- Walikuwa "*hawana Mungu*" (ms. 12). Nilikuwa sina Mungu.
- Walikuwa "hawana Baba mbinguni."
- Walikuwa "*hawana Kristo*" (ms. 12); unapokuwa huna Kristo "*huna amani*" (ms. 14). Unapokuwa huna Kristo, unakuwa huna tumaini (ms. 12). Hapa nilikuwa sina amani, tumaini. Nilijiuliza mara nyingi; kwamba nifanye nini?

Katika 1993 nilikutana na mhubiri kutoka katika kanisa la mitume jipya. Aliniambia kuhusu Yesu Kristo. Niliamini na kuungana na dhehebu hili. Nili "batizwa" kwa kunyunyuziwa maji.

“Uzao Mpya”

Yesu alidai kwamba njia ya kuingia katika Ufalme wake inapaswa kuwa pia uzao. Katika maongezi yake na Nikodemo, Yesu alisisitiza umhimu wa uzao mpya (Yoh. 3:1-5).

Mwaka huo uo, 1993, nilikutana na ndugu Boaz, ndugu Laban Ambogo na wamisionari wengine kutoka Marekani sehemu fulani karibu na Butere Magharibi mwa Kenya. Kwa mara ya kwanza nilisikia kuhusu Yesu Kristo. Niliamini nilichohubiriwa. Nikabatizwa katika siku hiyo katika maji mengi. (Mdo. 2:41; Yoh. 3:23). Katika Mdo. 2:42, Biblia inasema “*Walidumu katika fundisho la Mitume na katika ushirika.*” Nilikuwa na furaha sana kwa sababu swali langu “Nifanye nini” lilijibiwa. Sasa kulikuwa na swali linginge, “Nifanyeje ili niishi maisha ya Kikristo?” ilikuwa ni hamu yangu kufundisha na kuhubiri neno la Mungu kwa watu wengine. Swali langu pia lilijibiwa na Biblia. Nasoma katika 2 tim. 2:15, Biblia inasema, “*Jionyeshe kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukifundisha kwa halali neno la kweli.*” Naitaji mtu anifundishe. Nilikutana na waalimu kutoka W. B. S Nakuru nilipohamia hapa baada ya mwaka mmoja. Wakanipa baadhi ya masomo kumi na nne yote ambayo ambayo nilimaliza. Alafu nikatuma maombi katika shule ya Biblia kimataifa Afrika Kusini. Nikawa mwanafunzi katika shule hiyo ambapo nilisoma kupitia masomo ya mtandaoni hadi nikamaliza.

Toka wakati huo nimemtumikia Bwana wangu katika makusanyiko tofauti Nakuru.

Kanisa la kwanza kuhudumu lilikuwa Kanisa la Kristo Nakuru Mjini. Kupitia juhudi zangu na ndugu Benjamin Ronoh, tulianzisha Kanisa la Kristo Barut. Ndugu Humphrey Egesa ambaye baadae aliungana nasi alisaidia katika kazi ya uinjilisti. Ndugu Alphonce Kipngetich ni kijana kiongozi sawa na mwinjilisti.

Kwa miaka hiyo yote, tuliamini kwamba chochote tulichofanya kilikuwa kulingana na maandiko. Baadae katika mwaka wa 2011 wageni wanne walifika kutoka Tanzania. Walikuwa ni ndugu Boaz Auma, Ndugu Laban Ambogo, Ndugu Ellis Forsman (kutoka Marekani) na Rispa, mke wa Boaz. Ujio wao ulikuwa ni sehemu ya kugeukia, hasa kwangu. Nilisikia kuhusu makanisa ya Bwana yaliyotumia kikombe kimoja katika meza ya Bwana. Lakini hakuna mtu aliyewahi kuja na kufundisha kama Ellis alivyofundisha. Tulibadilika katika matumizi ya kikombe kimoja kulinga na kile kinachofundishwa katika Biblia. Shukrani kwa Bwana aliyetoa nafasi kwa ndugu Ellis kuja Afrika Mashariki. Mungu mbariki Ellis.

Maisha ya Kikristo ni kukazana. Sote tunatakiwa kukazana ili tuwe bora na sio wabaya. Mtume Paulo anatusihi, “Bali kwanza niliwahubiri

wale wa Dameski na Yerusalemu, na katika nchi yote ya Uyahudi, na watu wa mataifa, kwamba watubu na kumwelekea Mungu, wakitenda matendo yanayopatana na kutubu kwao." (Mdo. 26:20).

"Uzao wa Ajabu"

Uzao wa tatu na mwisho ni uzao wa ajabu. Yesu ni, "*Mzaliwa wa kwanza katika wafu*" (Kol. 1:18); kufufuka katika wafu kunaongelewa kama uzao. Kuna maswali matatu ambayo nimekuwa nikijiuliza binafsi:

- Nilitokea wapi?
- Ninafanya nini hapa?
- Ninakwenda wapi?

Tayari nimeshajibu maswali matatu. Biblia inatoa jibu kwa swali la tatu. Mtume Yohana aliandika, "Msistajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja amabayo watu wote waliomo makaburini watasikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu." (Yoh. 5:28-29).

Hivyo basi, Biblia ambalo ndilo neno la Mungu inanipa uhakika kwamba kuna maisha zaidi ya ulimwengu huu. Maisha zaidi (maisha baada ya kufa) inaleta maana katika maisha kabla ya kufa. Kama hakuna maisha baada ya kufa, basi maisha katika dunia hii haina maana. Tunapaswa tu kula, kunywa, na kupata kilekilichopo tunacho paswa kuwa nacho (1 Kor. 15:12-19).

Hivyo, ninakukaribisha katika kanisa la Kristo, ili tusafiri pamoja katika maisha ya kimbingu. Fanya yafuatayo:

- Sikia injili (Rum. 10:17)
- Amini injili (Yoh. 3:16; Mdo. 8:37)
- Tubu dhambi zako (Luka 13:3; Mdo. 17:30-31)
- Kiri jina la Yesu Kristo (Rum. 10:10)
- Batizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako (Mdo. 2:38; 8:38; 22:16).

Sasa wewe ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, mwana wa Mungu. Fanya yafuatayo ili uishi katika Kristo:

- "*Kaeni ndani yangu.*" Haitoshi tu kuanza. Yesu alisema, "*Yeyote asipokaa ndani yangu, hutupwa nje...*" (Yoh. 15:16). Ili kuzaa matunda na kumpendeza Mungu ni lazima tuwe waaminifu hadi mwisho wa maisha yetu, au hadi mwisho wa wakati (Ufu. 2:10)

- "*Lala katika Bwana*". "*Ni heri wafu wafao katika Bwana*" (Ufu. 14:13). Mungu atakuja pamoja na wale waliolala katika Yesu (1 Thes. 4:14). Nani asingependa kuwa Mkristo na kufurahia baraka ambazo hupatikana tu ndani ya Kristo? Kuwa mkristo. Kuwa mshiriki wa kanisa lake.

John Kombo Nandwa

Kanisa La Kristo Baruti

Nakuru, Kenya